**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA

# MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI [*THE PROPOSED ELECTORAL COMMISSION) BILL, 2023]*

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(5 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023)]*

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P 941,
**40490 Tambukareli**
**DODOMA.**

**30 Januari, 2023**

# YALIYOMO

*Ukurasa*


1.0 UTANGULIZI ..... 1

1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea ..... 1

1.1.1 Maelezo ya Awali ..... 1

1.1.2 Hadidu za Rejea ..... 2

1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada ..... 4

1.2.1 Upokeaji wa maoni ya Wadau ..... 4

1.2.2 Namna Kamati iliendesha vikao vya upokeaji wa maoni (*Public hearings*) ..... 5

1.3 Hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wadau ..... 8

2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA ..... 39

1.1 Utangulizi ..... 39

2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI ..... 42

2.1 Maelezo ya Utangulizi ..... 42

2.2 Marekebisho ya Jina refu ..... 42

2.3 Marekebisho katika Ibara ya 5 na Ibara ya 10 ya Muswada ..... 43

2.4 Marekebisho ya Ibara ya 7 ya Muswda ..... 44

2.5 Marekebisho ya ibara ya 8 ya Muswada ..... 44

2.6 Marekebisho ya Ibara ya 9 ya Muswada ..... 45

2.7 Marekebisho ya Ibara ya 16 (2) ya Muswada. ..... 46

2.8 Kuhusu Ibara ya 11 ya Muswada ..... 46

3.0 HITIMISHO ..... 48

3.1 Shukrani ..... 48

3.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja ..... 49

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI [*THE PROPOSED ELECTORAL COMMISSION) BILL, 2023]***

---

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

### 1.1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na tatu, kikao cha kumi kwenye Bunge la 12, tarehe 10 Novemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala,

Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.1.2 Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa msingi wa Miswada hii ni Falsafa ya 4R za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ambazo ni Maridhiano (*Reconciliation*), Ustahimilivu (*Resiliency*), Mabadiliko (*Reforms*) na Kujenga upya (*Rebulding*).

**Mheshimiwa Spika**, Falsafa hizi ni mkakati mahususi wa uongozi wa Rais unaolenga kuimarisha utawala bora, demokrasia na uchumi nchini, kwa kufungua milango ya mazungumzo na wadau mbalimbali wa kisiasa, kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa, asasi za kiraia na sekta binafsi. Aidha, Falsafa hii inalenga **kupitia upya sera na sheria** zinazohusu masuala muhimu kama vile siasa, afya, elimu, uwekezaji, biashara, usalama ikiwa ni pamoja na kujenga uhusiano mzuri na nchi jirani, wadau wa maendeleo na jumuiya za kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, wakati serikali ikiwasilisha miswada hii kwa kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala Katiba na Sheria, ilieleza kuwa **maudhui** ya Miswada yanatokana na Taarifa ya Kikosi Kazi kilicho undwa na Mheshmiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuboresha mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini. Aidha, maudhui mengine yametokana na mijadala mbalimbali kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini iliyofanyika mara kwa mara kupitia Jukwaa la Vyama Siasa na Kituo Cha Demokrasia Tanzania (Tanzania Centre for Democracy -TCD). Kwa muktadha huo, sheria hizi zimekusudia kutoa majawabu ya baadhi ya hoja zilizo jitokeza kwenye Taarifa ya Kikosi Kazi na kwenye Mijadala mbalimbali ya Siasa na Demokrasia nchini, kupitia jukwaa la Vyama vya Siasa na TCD.

**Mheshimiwa Spika**, katika muktadha huo, miswada hii mitatu inakusudia kuleta mapinduzi (reforms) za kisheria na kimfumo katika uchaguzi ili kupanua demokrasia nchini kwa kuongeza uhuru wa Tume ya Uchaguzi, Kuboresha usimamizi wa Uchaguzi na kuongeza ushiriki (inclusion) wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye uchaguzi. Miswada hii ya Sheria imekusudia kufanya Mfumo wetu wa Uchaguzi

kuwa **jumuishi zaidi** na wa **wazi zaidi, haki zaidi, na wenye usawa zaidi**.

## 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 5 Januari, 2024 ili kupokea maelezo ya Mhe. Jenista Joakim Mhagama, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

### 1.2.1 Upokeaji wa maoni ya Wadau

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) na 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mikutano ya kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearings*) kwa siku nne kuanzia tarehe 6, 8 hadi 10 Januari, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Miswada minne iliyofanyiwa kazi na Kamati hii, Ambayo ni: -

a) Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, wabunge na Madiwani wa mwaka 2023;
b) Muswada wa Sheria wa tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023;

c) Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa Mwaka 2023 [*The Political Parties Affairs Laws* (*Amendments) Bill, 2023*]; na
d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 [*The Written Laws* (*Miscellaneous Amendments*) *Bill, 2023*].

### 1.2.2 Namna Kamati iliendesha vikao vya upokeaji wa maoni (*Public hearings*)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata heshima ya kupokea watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao walijitokeza na kutenga muda wao kwa ajili ya jambo hili la maana kubwa kwa taifa letu, Kamati ilihakikisha kuwa kila sauti ilipewa nafasi yakusikilizwa kwa dhamira ya kuhakikisha Sheria tunazokusudia kuzitunga kwa niaba ya Watanzania zinawakilisha maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kusikiliza, kujifunza na kuyachukua maoni ya wadau wote kwa uzito unaostahili, kwa lengo la kufikia maamuzi ambayo yataleta mabadiliko chanya katika Miswada iliopo mbele yetu. Kwa muktadha huo, Kamati ilitenga muda wa dakika thelathini kwa taasisi za Kidini kutoa maoni na nasaha kuhusu Miswada, dakika ishirini kwa vyama vya siasa, dakika kumi kwa taasisi na asasi za kiraia na dakika

tano kwa wachangiaji binafsi. Hata hivyo, kwa wale ambao hawakuweza kumaliza michango yao kwa muda uliopangwa, Kamati iliwasihi kuwasilisha michango yao kwa maandishi ili iweze kufanyiwa kazi na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Miswada iliyofanyiwa kazi na Kamati na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

1) Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC) - Ujumbe ulioongozwa na Mhasham Baba Askofu Jude Thaddeus Rwaichi;
2) Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) – Ujumbe ulioongozwa na Askofu Dkt. Fredrick Shoo aliyekuwa Mkuu wa Kanisa la Kilutheri Tanzania na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania;
3) Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu Tanzania - Ujumbe ulioongozwa Sheikh Mussa Yusuph Kundecha;
4) Taasisi na Asasi za Kiraia 31 zilizoshiriki kwenye majadiliano na zingine zaidi ya 400 zilizotuma kwa maandishi maoni na mapendekezo yao; pamoja na

5) Wadau binafsi 1707 waliopata fursa ya kushiriki katika mikutano ya kupokea maoni kutoka maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 25 Januari, 2024 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 1.3 Hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wadau

**Mheshimiwa Spika**, Wakati Kamati ilipokutana na Wadau hoja 38 ziliibuliwa na Wadau kama ifuatavyo: -

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| [redacted] | [redacted] | | |
| LHRC, TLS, Twaweza, CSL, JUKATA na Jamii Forums | **Jina refu** | Kurekebisha jina refu lisomeke“Sheria kwa ajili ya kufafanua utaratibu wa kuweka mfumo uliyo wazi, shindanishi na shirikishi na kuweka utaratibu wa uendeshaji wa vikao vya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na kuweka masuala mengine yanayohusiana nayo”. | Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kiwe ndiyo chombo pekee kinachosimamia chaguzi zote nchini, zikiwemo Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
| --- | --- | --- | --- |
| ACT WAZALENDO,LHRC, TLS, Twaweza, CSL, JUKATA na Jamii Forums u | **Ibara ya 1,3 na 4** | Kuongeza neno” **huru**” mara baada ya neno” Tume” ili isomeke **Tume huru ya Uchaguzi”.** | Kuongeza neno “huru.” kwenye jina la Tume kutasaidia kueleza umuhimu wa chombo kinachoshughulikia uchaguzi kuwa huru, kisidhibitiwe na serikali, vyama vya siasa, taasisi au mtu mwingine yeyote. Pia kuhakikisha uhuru wa Tume na maamuzi yake kupingwa Mahakamani. |
| TEC | **Ibara ya 1** | Kubadili jina la Tume kuwa “TUME YA UCHAGUZI YA JAMHURI YA MUUNGANO”. | Kuendana na Ibara ya 74 ya Katiba ya JMT 1977. |
| LHRC, TLS, Twaweza, CSL, | | Sheria iwe kamilifu isomke “Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, 2023”. | Muswada huu uweze kusimamia chaguzi mbalimbali ikiwemo |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| JUKATA na Jamii Forums | | | uchaguzi wa uwakilishi wa nafasi ya ubunge katika Bunge la Afrika (PAAP), EALA na nafasi nyingine. |
| LHRC, TLS, Twaweza, CSL, JUKATA na Jamii Forums | | Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Taifa ya Uchaguzi 2024, na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri atatangaza kwa notisi katika Gazeti la Serikali ndani ya siku sitini (60) tangu Rais alipotia saini. | Kuhakikisha kuanza kwa sheria kuanza kutumia mapema iwezekanavyo mara baada ya kupitishwa na Bunge. |
| LHRC, TLS, Twaweza, CSL, JUKATA na Jamii Forums, BAVICHA, NCCR – MAGEUZI, TEC | **Ibara ya 5** | (a) Ibara ya 5(1) kiweke sharti kwa nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyeki kupatikana kupita Kamati ya Usaili. | Kuweka dhana ya uhuru wa Tume, kwa kuweka sharti la Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti kufanyiwa usaili na Kamati ya Usaili. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
| --- | --- | --- | --- |
| | | | AU<br><br>Mbadala wake, ni kuwapa mamlaka wajumbe wa Tume kuchagua viongozi wao yaani Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti. |
| TEC | | (b) Wajumbe wa Tume wasiteuliwe na Rais na badala yake kuwe na chombo huru cha uteuzi wa wajumbe na waape mbele ya jaji wa mahakama kuu au mahakama ya Rufaa. | Kuhakikisha Tume inakuwa Huru |
| LHRC, TLS, Twaweza, CSL, | | Kuongeza kifungu kipya kitakachoweka sharti la kuzingatia | Kuweka takwa la kuzingatia jinsia. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| JUKATA na Jamii Forums, TGNP, | | jinsia kwa nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti.<br>Kifungu kipya 5(4), kisomeke; Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5 uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti utazingatia jinsia. | |
| UMOJA WA ASASI ZA VIJANA, TAASISI YA TUSONGE | | Uteuzi wa Mwenyekiti na makamu mwenyekiti wa Tume, kamati za usaili na uchunguzi uzingatie vijana. | Kutoa nafasi ya vijana katika Tume na Kamati zake |
| CHADEMA | | Katika muundo wa Tume kuwe na uwakilishi wa vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni. | Kuhakikisha uwazi katika mchakato wa uchaguzi |
| MASHIRIKA YA VIJANA (TYVA, TBI, TYC, BFC, | | (1) Kifungu kiboreshwe kwa kuongeza kifungu kingine kitakachoweka sharti kwa Rais | Kifungu hakijatoa nafasi ya uwakilishi wa makundi maalumu |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| ZAFAYCO, RESTLESS DEVELOPMENT, YPC, YOWDO, ADD INTERNATIONAL na YUNA TANZANIA) | | kuteua wajumbe wa Tume kwa kuzingatia makundi maalumu ambayo ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. | |
| ADC | Ibara ya 6 | **Ibara ya 6(1)**<br>(1) Mamlaka ya uteuzi wa wajumbe wa Tume yaondolewe kwa Rais.<br>(2) Mwenyekiti na makamu mwenyekiti apishwe mbele ya Bunge. | Rais ni Mwenyekiti wa Chama hivyo Rais kuteua wajumbe inaondoka maana ya Tume Huru |
| TANLAP | | Kuongeza kifungu kitakacho anzisha tume Huru ya Usuluhishi wa migogoro ndani ya vyama vya | Hakuna tume Huru ya usuluhishi wa migogoro ndani ya vyama vya siasa kabla ya kupeleka kesi |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| | | siasa kabla, wakati na baada ya uchaguzi. | Mahakamani. Tume itasaidia kudumisha amani |
| TANLAP | | Kiongezwe kifungu kipya kitakachotoa sharti kuwa, maamuzi ya Tume yanaweza kupingwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania endapo yatakuwa yanakiuka Katiba na Haki za Binadamu na yametolewa visivyo halali (aliyetoa amekiuka madaraka au mamlaka yake). | Uhuru wa maamuzi ya Tume uwe na kikomo au exception maana inaweza kutoa maamuzi ambayo si sahihi. |
| TEC | | **Ibara ya 6(3)**<br>Kirekebishwe ili kuondoa takwa la Tume kumtaarifu mwanasheria mkuu wa serikali pale inaposhitaki au kushitakiwa. | Tume iwe huru kuendesha mashtaka yake kama ilivyoshitakiwa na watu mbalimbali. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
| --- | --- | --- | --- |
| | | | |
| TEC | **Ibara ya 7** | Ibara ya 7 (1) Kuongeza sifa ya elimu na uadilifu kwa wajumbe wa Tume na kwamba wawe na elimu ya juu kutoka chuo kinachotambulika na serikali. | Kuhakikisha Tume inakuwa na weredi. |
| BAVICHA | | **Ibara ya 7 (1)**<br><br>**Kufuta Ibara ya 7(2)** | Sifa za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume zimeainishwa katika Ibara ya 74(1)(d) ya Katiba. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| ACT WAZALENDO, TANLAP, WILDAF, ALIFU AZANI,LHRC, TLS, TWAWEZA, CSL, JUKATA na Jamii Forums, TEC<br><br>TLS | | **Ibara ya 7(1)**<br>(a) Kuongeza sifa ya mjumbe wa Tume ya kutokuwa mwanachama wa chama chochote na asiwe amewahi kushiriki mchakato wowote wa siasa.<br><br>(b) Kufuta sifa ya mtu kuwa wakili katika uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume. | ili iendane na ibara ya 74(4) ya katiba ya JMT 1977.<br>Na kuhakikisha kuwa Tume inakuwa huru na kuepuka upendeleo.<br><br>Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume watapaswa kuwa ni Majaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani. |
| GODWIN GONDE | **Ibara ya 7(2)(d)** | Kufuta aya (d) | Sifa zijulikane badala ya kuacha sifa yoyote ambayo hijulikana. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| JUKWAA LA VIJANA WACHAMBUZI na MASHIRIKA YA VIJANA (TYVA, TBI, TYC, BFC, ZAFAYCO, RESTLESS DEVELOPMENT, YPC, YOWDO, ADD INTERNATIONAL na YUNA TANZANIA) | | Katika sifa za uteuzi wa wajumbe iongezwe sifa ya umri kuanzia miaka 21 hadi 35. | Kutoa nafasi kwa vijana kushiriki kuwa wajumbe wa Tume. |
| TEC | | Kuongeza kifungu kipya; "Awe na elimu angalau shahada ya kwanza". | |
| FOUNDATION FOR DISABILITY | **Ibara ya 7** | Kuwepo na nafasi ya watu wenye ulemavu katika shughuli za Tume | Kuwa na uwakilishi wa watu wenye ulemavu. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
| --- | --- | --- | --- |
| | | kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya chini. | |
| CPA George Fumbuka,<br>Chama cha NRA | **Ibara ya 8** | (a) 8(1) Mjumbe wa Tume atashika nafasi ya madaraka kwa kipindi cha mihula minne (4) ya miaka kumi kumi (yaani hadi miaka 20) hadi atakapostaafu au kile kitakachofika kwanza. | Ili kulinda nafasi yake (TENURE SECURED) aweze kutimiza wajibu wake. |
| TEC, CCT | | (b) 8(2)e(ii)<br>Neno" **tabia mbaya"** lipewe tafsiri | Tabia mbaya ni neno pana na linaweza Kuleta mkanganyiko Katika matumizi yake. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| TEC | | (c) 8(3)<br>Mamlaka ya Rais kuunda Tume ya uchunguzi itakayomshauri ipasavyo kumuondoa mjumbe wa Tume iwe ni ya lazima. | Kifungu kilivyo kinatoa hiari kwa Rais kuunda Kamati jambo ambalo linaathiri uhuru wa Tume. |
| TEC<br><br>TREE OF HOPE | | (d) Ibara ya 8(4). Kuundwe Kamati huru ya uchunguzi na itakayo mshauri Rais ipasavyo wakati kumuondoa mjumbe wa Tume yenye mchanganyiko wa wadau kutoka sekta mbalimbali kama vile vyama vya siasa, viongozi wa dini, sekta binafsi, asasi za Kiraia na Serikali.<br><br>(e)Uteuzi wa wajumbe uzingatie usawa wa kijinsia. | Wajumbe wa Tume wote ni wateule wa Raisi. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| ACT WAZALENDO, TANLAP | **Ibara ya 9(1)** | kuongeza Wajumbe 2 kwenye Kamati ya Usaili kutoka vyama vya siasa vyenye uwakilishi bungeni na Asasi za kiraia. | Kuhakikisha mchakato wa usaili kufanyika kwa uwazi na usawa. |
| JUKWAA LA VIJANA WACHAMBUZI | **Ibara ya 9(2)** | Katika sifa za uteuzi wa wajumbe iongezwe sifa ya umri kuanzia miaka 21 hadi 35. | Kutoa nafasi kwa vijana kushiriki kuwa wajumbe wa Tume. |
| THABITI MRANGI | **Ibara ya 9** | Kufuta Ibara ya 9 ili kusiwe na Kamati ya Usaili badala yake Rais aachiwe mamlaka ya kuteua wajumbe wa Tume. | Kusaili kisha kumpelekea Rais majina ili ateue ina dogosha nafasi ya Rais na kuvunja Katiba Ibara ya 31 kuhusu uhuru wa Rais. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| LHRC, TLS, TWAWEZA, CSL, JUKATA, Jamii Forums | **Ibara ya 9(3)** | (a) Hakuna mtaalam wa masuala ya ajira kwenye muundo wa Kamati ya Usaili. Tunapendekeza marekebisho ya kifungu hiki kisomeke; "Mjumbe mmoja kutoka kwenye Sekretariat ya ajira kwa kuzingatia jinsia".<br><br>(b) Mkurugenzi wa Uchaguzi asiwe Katibu wa Kamati ya Usaili badala yake Katibu wa Kamati ya Usaili awe Katibu wa Bunge au Mtendaji wa Mahakama au Mkurugenzi wa Tume ya Haki za Binadamu.<br><br>(c) Wajumbe wa Kamati ya Usaili waongezwe wawe tisa, kwa | Ili kuleta utaalamu kwenye Kamati ya Usaili.<br><br>Kuepuka mgongano wa maslahi kwa kuwa Wajumbe wa Tume ni maboss wake kwani Mkurugenzi huteuliwa baada ya kupendekezwa na Tume. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
| --- | --- | --- | --- |
| | | kuongeza uwakilishi kutoka viongozi wa dini, na Asasi za Kiraia kwa kuzingatia uwakilishi wa makundi wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu. Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya uchaguzi asiwe katibu wa Kamati ya Usaili, bali Katibu wa Bunge. | |
| LHRC, TLS, Twaweza, CSL, JUKATA, Jamii Forums, TAMWA, Arif Noorally | **Ibara ya 9(3)** | (a) Majina ya wajumbe kupelekwa Bungeni kwa ajili ya vetting. Tunapendekeza kifungu hiki kirekebishwe na kisomeke kama ifuatavyo; Rais atateua | Ili kuongeza ushiriki wa Bunge katika mchakato wa upatikanaji wa wajumbe wa Tume. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
| --- | --- | --- | --- |
| Fazel, Dkt. Denis Mchunguzi | | Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kutoka miongoni mwa majina yaliyowasilishwa kwake na kamati ya usaili na atawasilisha majina hayo bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge.<br><br>Endapo Bunge litakataa jina lolote, majina au orodha ya majina, kwa kutoa sababu, mchakato wa usaili utaanza upya kwa jina, majina au orodha iliyokataliwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki. | |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| | | Katika Ibara ya 9 (6) na 9 (8)- Kuwapata wajumbe wa Tume kuzingatie jinsia. | Kuweka usawa wa jinsia katika Tume. |
| TAMWA, TREE OF HOPE | **9(6)** | Kuwe na usaili wa wazi wa kuwapata wajumbe wa kamati ya usaili ili kuwawezesha wananchi kutoa maoni yao juu ya wajumbe wa Tume. | Kuongeza Imani ya wananchi kwa Tume huru ya uchaguzi. |
| TAMWA, TREE OF HOPE | **9(8)** | Walifaulu kwa viwango vya juu ndio wapelekwe kwa Rais na Rais azingatie viwango vya ufaulu na uzoefu kutoka kwa Kamati ya Usaili. Hivyo, Raisi awe anathibitisha majina ya wajumbe wa Tume yaliyopendekezwa na Kamati ya usaili au aweze | Ili kuwafanyia haki walioshiriki katika usaili na kupata wajumbe wenye weredi. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| | | kuamuru mchakato kuanza upya iwapo atabaini kuwepo kwa dosari. | |
| ACT WAZALENDO, LHRC, TLS, TWAWEZA, CSL, JUKATA, Jamii Forums na CHADEMA | **Ibara ya 10** | Mwenyekiti na Makamu mwenyekiti wa Tume wapatikane kwa njia ya Ushindani, Hivyo kiongezwe kifungu 10(2) kitakachoeleza kuwa katika kutekeleza mamlaka yake kwa mujibu wa 10(1) Rais atateua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kutoka miongoni mwa majina 3 kwa kila nafasi yaliyopendekezwa na Kamati ya Usaili. | Wajumbe wana hadhi sawa kutofautisha njia ya upatikanaji italeta matabaka hivyo Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru uwe ushindani miongoni mwa watu wenye sifa zilizotajwa katika Kifungu Cha 7(1).<br><br>Kuweka dhana ya uhuru wa Tume, kwa kuweka sharti la Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kufanyiwa usaili na |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
| --- | --- | --- | --- |
| | | | Kamati ya Usaili/kamati ya uteuzi. Mbadala wake, ni kuwapa mamlaka wajumbe wa Tume kuchagua viongozi wao yaani Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti. |
| TANLAP | | Usawa wa Kijinsia uzingatiwe katika uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.<br><br>Vilevile, Sheria itamke kuwa Waziri mwenye dhamana atatunga kanuni za kuwezesha upatikanaji wa wajumbe utakaozingatia usawa wa kijinsia. | Usawa wa kijinsia haujazingatiwa katika uteuzi wa wajumbe wa Tume. |
| | | | |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| LHRC, TLS, TWAWEZA CSL, JUKATA na Jamii Forums | **Ibara ya 11** | (a) Kufuta na kuandika upya kifungu cha 11(1) kuhusu Majukumu ya Tume kama ifuatavyo;<br>i. Uandikishaji wa wapiga kura.<br>ii. Kusimamia na kuratibu uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani, Serikali za Mitaa.<br>iii. Kutoa na kuratibu elimu ya mpiga kura.<br>iv. Kuainisha majimbo ya uchaguzi.<br>5. Kusimamia na kuratibu kura ya uamuzi.<br><br>(b) Kurekebisha kifungu 11(2) ili kuainisha majukumu ambayo Tume inaweza kukaimisha kwa | Ili kuendana na majukumbu yaliyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br><br>Kutoleta makanganyiko wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Tume. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| | | Mkurugenzi wa Uchaguzi au Mtumishi au Mtendaji wa Tume. | |
| BAVICHA | | (c) Katika Ibara ya 11(1)(c) vigezo vya kugawa majimbo vitakavyotumiwa na Tume viainishwe katika sheria | |
| TEC | **13 (1-6)** | Sheria itamke kuwa maamuzi yanayofanyika nje ya vikao ni batili. | Sheria inaelekeza maamuzi ya Tume yafanyike kwenye vikao. |
| TEC | **15** | Kura ya mwenyekiti ya turufu ibadilishwe na kuitwa kura ya ziada. | Kura ya Turufu ni kura ya kupindua maamuzi. |
| LHRC, TLS, TWAWEZA CSL, JUKATA na Jamii Forums | **Ibara ya 16** | Kurekebisha kifungu cha 16 ili kuweka sharti la Tume kutumia miongozo yake katika masuala ya fedha. Isomeke:<br>“Wajumbe wa Tume watalipwa | Ili kuongeza uhuru wa Tume. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| | | posho na stahili nyingine kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya Tume." | |
| | | Tume iwe na watumishi wa kudumu na sio wa muda | Kulinda uhuru wa Tume katika kutekeleza majukumu yake |
| ACT WAZALENDO, NCCR MAGEUZI | **Ibara ya 17** | Itambue Katiba ya Zanzibar. | Ibara inatambua Katiba ya 1977 ni vema ikatambua Katiba ya Zanzibar. |
| | | (a) Wakurugenzi wa Uchaguzi wasiteuliwe na Rais bali wapatikane kwa ushindani kupitia usaili. | Mchakato wa kumpata Mkurugenzi wa Tume ya uchaguzi kuwa wazi kwa kuruhusu mtu yeyote kuomba kulingana na sifa zilizoainishwa katika Ibara ya 18(2) na kusailiwa kupitia kamati ya Usaili. |
| ACT WAZALENDO, NCCR MAGEUZI | **Ibara ya 18** | (a) Ibara ya 18(1) ifanyiwe marekebisho ili Rais ateue | |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| | | Mkurugenzi kutokana na Majina 3 yaliyoletwa na Kamati ya Usaili.<br><br>(b) Ibara ya 18(2) irekebishwe kwa kufuta aya (d) inayotaka Mkurugenzi awe afisa mwandamizi katika utumishi wa umma.<br><br>(c) Ibara ya 18(2) kuongeza Sifa za Mkurugenzi wa uchaguzi kuwa ni:<br><br>(1) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Sheria ya UraiaTanzania;<br>(2) awe ni mtu mwaminifu na mwadilifu; | Aidha, kuondoa dhana ya ubaguzi kwa watanzania wote, pia wale wanaofanya kazi katika sekta binafsi au umma. Kifungu hiki kinakiuka Ibara ya 13 (1) & (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayohusu usawa mbele ya sheria. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| | | (3) awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa kwa mujibu wa sheria;<br>(4) Awe na uzoefu katika uongozi, utawala au masuala ya uchaguzi<br>(5) Asiwe mwanachama wa chama chochote cha siasa au kufungamana na chama chochote cha siasa.<br>(6) Asiwe amewahi kushiriki mchakato wowowte wa Kisiasa; na<br>(7) sifa nyingine ambayo Kamati ya Usaili itaona inafaa ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Tume.<br>(8) Asiwe ametiwa hatiani kwa makosa yoyote ya unyanyasaji wa kijinsia. | |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| LHRC, TLS, TWAWEZA CSL, JUKATA na Jamii Forums | | (d) Kurekebisha Kifungu cha 18 ili kuondoa sifa ya Mkurugenzi ya kuwa raia wa kuzaliwa na lazima ya kuwa mtumishi wa umma. Kisha kuweka sifa ya raia wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Tanzania". | Kuondoa ubaguzi watu wasiyofanya kazi kwenye utumishi wa umma na wanasifa na vigezo. |
| TEC na ACT WAZALENDO | **18 (2)d** | Kuondoa sifa ya Mkurugenzi kuwa afisa mwandamizi katika utumishi wa umma. | Inaminya wigo wa sifa za upatikanaji wa mkurugenzi wa uchaguzi, wigo huo utanuliwe kwa maana kamati ya usaili itazingatia ufaulu na uzoefu hivyo isilazimu kuwa mtumishi wa umma. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| LHRC, TLS, TWAWEZA CSL, JUKATA, Jamii Forums na NCCR MAGEUZI | **Ibara ya 20** | Fedha za uendeshaji wa shughuli za Tume zitoke katika Mfuko Mkuu wa Hazina. | Kuwa na uhakika wa rasilimamali fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. |
| LHRC, TLS, TWAWEZA CSL, JUKATA na Jamii Forums | **Ibara ya 20 (4)** | Kurekebisha kifungu hiki kwa kuondoa neno watumishi wa umma. Hivyo kisomeke; Mkurugenzi wa Uchaguzi atatekeleza majukumu yake kwa kusaidiwa na watendaji ambao wataajiriwa na Tume au watu wengine wenye sifa kwa kadri itakavyohitajika. | Kuleta dhana ya uhuru wa Tume, ni muhimu kwa Tume kutumia wafanyakazi wake. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| TEC, ACT WAZALENDO, BAVICHA, LHRC, TLS, TWAWEZA CSL, JUKATA na Jamii Forums | **20** | Mkurugenzi wa Tume awe ni mkuu wa sekretarieti ya watumishi wa Tume na si watumishi watakaotoka nje ya Tume. | Kuhakikisha Tume inakuwa Huru. |
| TEC, ACT WAZALENDO, BAVICHA, LHRC, TLS, TWAWEZA CSL, JUKATA na Jamii Forums | **21** | Kuondoa dhana ya Tume ya kuazima watumishi katika kutekeleza majukumu yake. | Kuwezesha watumishi wa Tume kuwajibika kwa Tume na kuchukuliwa hatua endapo watakosa uaminifu na uadilifu kwa Tume. |
| TEC, ACT WAZALENDO, BAVICHA, LHRC, TLS, TWAWEZA CSL, JUKATA na Jamii Forums | | Kuongeza kifungu kipya ambacho kitaweka takwa wakati wa kuajili watumishi wa tume, Mkurugenzi atahakikisha asilimia 50 ya watumishi wa Tume ni vijana. | Kuongeza ushiriki wa vijana. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
| --- | --- | --- | --- |
| TEC | 22 | Kuwe na mfuko maalaumu wa kugharamia shughuli za Tume. | Kuhakikisha Tume inakuwa Huru. |
| TEC, BAVICHA, BAWACHA na ACT WAZALENDO | | Fedha za kuendesha mfuko wa Tume zitoke kwenye mfuko mkuu wa serikali badala ya kutoka kwenye bajeti ya wizara. | Kuhakikisha Tume inakuwa Huru. |
| TEC | 23 | Kuondoa takwa la Tume kushauriana na Waziri wa utumishi katika kuunda Sekretarieti na badala yake Tume ianzishe idara, vitengo na sehemu katika utekelezaji bora wa shughuli zake. | Kujenga Imani ya Tume kwa wananchi. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| TAMWA | **Ibara ya 27** | Kuongeza kanuni na miongozo itakayotungwa chini ya kifungu 27 kuwa ni:<br>(a) Sera, na mpango mkakati wa kukuza ujumuishwaji wa makundi ya wanawake, vijana wa kike na wa kiume, na watu wenye ulemavu katika michakato ya uchaguzi.<br><br>(b) Sera na mpango mkakati huo uhakikishe fedha zitakazotengwa na serikali kwa ajili ya uchaguzi pia zinatumika katika kuboresha ushiriki wa wanawake, vijana na wenye ulemavu kwenye michakato ya uchaguzi. | Kuongeza wigo wa kanuni na miongozo itakayotungwa kusimamia masuala ya jinsia ndani ya vyama vya siasa. |

| MTOA HOJA | IBARA | MAONI NA MAPENDEKEZO | SABABU |
|---|---|---|---|
| | | (c) sera na mpango mkakati wa tume kujengewa uwezo wa kuratibu uchaguzi unaozingatia masuala ya kijinsia na kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia katika mchakato wa uchaguzi. | |
| CCM | | Kuongeza sura mpya kuhusu elimu ya mpiga kura na tume ipewe jukumu la kuandaa mtaala. | Kuweka utaratibu bora wa elimu ya mpiga kura. |
| [redacted] | [redacted] | | |

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchambuzi wa hoja hizo pamoja na maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika Muswada, baadhi ya changamoto zilizobainika utatuzi wake unahitaji mabadiliko ya Sheria zingine ambazo hazifanyiwi kazi na Kamati kwa sasa.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023 *The Proposed Electoral Commission) Bill, 2023*), ukiwa umegawanyika katika sehemu Tano na yenye jumla ya Ibara ishirini na nane (28) ambao unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo inalenga kuanzisha Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kubainisha Muundo wa Tume na kuainisha majukumu ya Tume na taratibu nyingine za uendeshaji wa Tume.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya kwanza ya Muswada inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Sheria inayopendekezwa kutungwa, mawanda ya matumizi, utaratibu wa kuanza kutumika pamoja na tafsiri ya misamiati mbalimbali kwa kadri ilivyotumika ndani ya Sheria inayopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu Uanzishwaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Muundo wa Tume, sifa za wajumbe wa Tume na muda wa utumishi wa wajumbe, posho na stahiki zao pamoja na uhusiano wa Tume ya Taifa Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Sehemu hii ya Muswada pia inahusisha masharti ya uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ambapo uteuzi wao utazingatia masharti yaliyopo katika Ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, katika sehemu hii, Muswada unapendekeza kuwepo kwa utaratibu wa usaili kwa nafasi za wajumbe wengine watano wa Tume, na pia sehemu hii inampa mamlaka Rais kuunda Kamati ya Uchunguzi ambayo itakua na jukumu la kufanya uchunguzi na kumshauri Rais iwapo itatokea suala la mjumbe kuondolewa kwenye nafasi yake.

**Mheshimiwa Spika**,Sehemu ya tatu ya Muswada inaanzisha Sekretarieti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuweka nafasi ya Mkurugenzi wa Uchaguzi na sifa za mtu anaestahili kuteuliwa kwenye nafasi hiyo na majukumu yake,Pia inaweka nafasi za watumishi na watendaji wengine wa Tume na kuweka sharti kwao kua watachukuliwa kama watumishi wa Tume kwa kipindi chote watakapokua wakitekeleza majukumu ya Tume na kwamba watapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya Sheria, taratibu na kanuni za utekelezaji wa majukumu ya Tume.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nne ya Muswada inahusu vyanzo vya mapato ya Tume ambayo yatatokana na bajeti ya serikali na Masharti ya matumizi

ya fedha za uendeshaji wa Tume kutoka kwenye mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile sehemu hii inamtaka Mkurugenzi wa Uchaguzi kutunza vitabu vya hesabu vinavyohusiana na Tume na kuandaa taarifa ya hesabu za mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma ambazo zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyo kwa Taasisi nyingine za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tano ya Muswada huu inahusisha Masharti Mengineyo ambapo inapendekeza Tume kupata Mamlaka ya kutengeneza kanuni, miongozo na maelekezo mbalimbali yatakayoiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ubora na ufanisi.

Aidha sehemu hii inapendekeza kuwepo kwa mashrti ya mpito ambayo yanamtaka mtu yeyote atakayeshika nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti au mjumbe wa Tume kushika nafasi hiyo hadi ujumbe wake utakapokoma.

## 2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa kiasi kikubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi wa maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu, Kamati inayo maoni ya jumla na mapendekezo mahsusi ambayo yakizingatiwa yatarahisisha mchakato wa utekelezaji wa Sheria hii kama ifuatavyo: -

### 2.2 Marekebisho ya Jina refu

**Mheshimiwa Spika**, Hadhi ya Tume katika Katiba Ibara ya 74(7) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kwamba Tume ni Idara Huru itakayotekeleza majukumu yake bila kuingiliwa na mtu yoyote au Taasisi yoyote. Kamati iliishauri Serikali kufanya maboresho ya jina la Tume ili kuendana na masharti yaliopo, Serikali ilikuwa na maoni kuwa kuongeza neon Huru kwenye jina la Sheria ni kubadili maudhui ya jina lililopo linalotokana na Ibara

ya 74(1) ya Katiba inayotambua kwamba Tume itakuwa ni Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa matumizi ya neno HURU hayakinzani na matakwa ya Katiba kwa kuwa Katiba haijaelekeza jina rasmi la kutumika na Tume kama ambavyo Katiba imeelekeza majina ya kutumia kwenye uwanzishaji wa Taasisi mbalimbali za Kikatiba mfano Ibara ya 112(1) na 129(1) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, 1977.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayopendekeza jina "Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi" litumike popote ilipotumika jina "Tume ya Taifa ya Uchaguzi".

### 2.3 Marekebisho katika Ibara ya 5 na Ibara ya 10 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Masharti yaliyopo katika Ibara ya 5 Ya Muswada yanazungumzia Muundo wa Tume ambao ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe watano (5) ambao watateuliwa na Rais, Ibara ya 10 inahusu Uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Tume.

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilikuwa na maoni kuwa masharti yaliyopo katika Ibara ya 5 na 10 yanafanana kimantiki kwa kuwa yote yanahusu uteuzi wa Wajumbe wa

Tume na kuapishwa kabla ya kushika madaraka hivyo tunashauri ilishauri kunganishwa kwa vifungu hivyo ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali mapendekezo na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati kuhusiana na mpangilio wa Ibara hizo.

### 2.4 Marekebisho ya Ibara ya 7 ya Muswda

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 7 ya Muswda inahusu Sifa za wajumbe wa Tume, na Ibara ya 7(2)(d) iainishe sifa ambazo zinakusudiwa kuongezwa, aidha, Ibara ya 7(2)(a) inafanya rejea ya Sheria ya Uraia Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikuwa na maoni kuwa jukumu la kuainisha sifa za wajumbe wa Tume libaki kwa Bunge pekee. Aidha, kamati iliishauri Serikali iandike sura ya Sheria inayoyerejewa kwenye maelezo ya pembeni (*Marginal Note*) ya Ibara ndogo ya 7(2)(a). Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati**.**

### 2.5 Marekebisho ya ibara ya 8 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika** Ibara ya 8(2)(e)(ii) ya Muswada imeweka sharti la maneno "tabia mbaya" kuwa ni miongoni mwa sababu zitakazopelekea mjumbe wa tume kuondolewa katika nafasi yake, Kamati iliona

matumizi ya maneno "tabia mbaya" yana tafsiri pana Kamati hivyo ni muhimu yakawekewa tafsirii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati yanayofafanua matumizi ya maneno "tabia mbaya" kwa muktadha wa Ibara hii.

## 2.6 Marekebisho ya Ibara ya 9 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Ibara 9(3) ya Muswada imemtaja Mkurugenzi wa uchaguzi kuwa ndiye atakuwa Katibu wa Kamati ya Usaili wa wajumbe wa Tume, Ibara ya 18(1) ya Muswada imeeleza kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa masharti ya upatikanaji wa Mkurugenzi wa Tume yanafuata baada ya kuwepo kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa msingi huo Kamati ilishauri Mkurugenzi wa uchaguzi asiwe Katibu wa Kamati ya Usaili na badala yake atafutwe mtu mwingine miongoni mwa Watumishi wa Umma waandamizi kwa cheo chake ama sifa alizonazo.

**Mheshimiwa Spika**, Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

## 2.7 Marekebisho ya Ibara ya 16 (2) ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika** maudhui ya Ibara hii yanaeleza kwamba wajumbe wa tume watalipwa Kiinua mgongo baada ya kumaliza kuhudumu nafasi ya ujumbe wa Tume.

**Mheshimiwa Spika** katika Ibara hii Kamati ilitaka Serikali kuweka wazi kuwa Wajumbe watume watalipwa kwanza mishahara ili wastahili kulipwa Kiinua mgongo kama ambavyo inavyopaswa kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya watumishi wa umma. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

## 2.8 Kuhusu Ibara ya 11 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, ibara ya 11 ya Muswada inaeleza majukumu ya Tume kuwa yatahusiana na uratibu na usimamizi wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na madiwani. Sheria haijajumuisha mapendekezo na maoni ya wadau ya kuitaka Tume iwe ndicho chombo pekee cha uzimamizi wa uchaguzi nchini, ikiwemo usimamizi wa chaguzi za serikali za Vijiji, Vitongoji na Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu ibara hii, serikali ilieleza kuwa uchaguzi wa Serikali za Vijiji, Mitaana Vitongoji unfanyika mwaka huu (2024) na tayari maandalizi yamekwisha fanyika, kwahiyo itakuwa vigumu kwa sasa kubadiri

majukumu ya usimamizi wa uchaguzi huu, na kwamba inaendelea kufanya utafiti juu ya namna bora ya kusimamia uchaguzi huo kwa siku za usoni. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato utakao wezesha kuwa na Chombo kimoja pekee cha kusimamia chaguzi zote nchini, ikiwemo uchaguzi wa Serikali za Vijiji, Mitaa na Vitongoji.

## 3.0 HITIMISHO

### 3.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb – **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe

20. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Jenista Joakim Mhagama, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga (Mb) Naibu Waziri wa Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga (Mb) Naibu Waziri wa Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Dkt. Jim Yonazi Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati Ndg. Frank Nkya, Ndg. Ganjatuni Kilemile na Ndg. Ndoh'no William Abel kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

## 3.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na Kamati pamoja na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

30 Januari, 2024